LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA • Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037,
E-mail: lhrc@humanrights.or.tz Website: www.humanrights.or.tz

for a Just and Equitable Society

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU AWAMU YA PILI YA KAMPENI YA KUSAMBAZA UELEWA WA RASIMU YA PILI (KAMPENI GOGOTA)

23 SEPTEMBA, 2014

Ndugu wanahabari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa mara nyingine tena kilifanya uzinduzi wa Kampeni yake Gogota ya kusambaza uelewa wa rasimu ya pili ya Katiba kwa wananchi. Awamu hii ya pili ya Kampeni Gogota ilizinduliwa rasmi tarehe 19 Agosti 2014 kwenye Ukumbi wa Sinema wa Mlimani City kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 7:00 mchana na mgeni rasmi akiwa Mhe. Joseph Butiku. Baada ya uzinduzi huo kufanyika Mlimani City, wafanyakazi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walitawanyika mikoani kwa ajili ya kutoa elimu ya rasimu ya pili ya Katiba. Kwenye uzinduzi huo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilizindua filamu iliyochezwa na wasanii mbalimbali yenye maudhui ya Katiba na kuhusianisha maisha ya kawaida na Katiba.

Ndugu wanahabari,

Kama tulivyowafahamisha hapo awali lengo la Kampeni Gogota ni kusambaza uelewa wa rasimu ya pili ya Katiba kwa wananchi na kuwahamasisha kushiriki katika mchakato hususani kufuatilia Bunge la Katiba na pia kupiga kura ya maoni kipindi kitakapofika. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilichukua jukumu hili la kutoa elimu ya rasimu ya pili ya Katiba na mchakato kwa wananchi baada ya kuona tangu Rasimu ya pili ya Katiba imetoka, wananchi waliacha kabisa ajenda ya Katiba wakiona kuwa mchakato umekamilika.

Katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu kuhusu Katiba mpya, kituo kimetumia nyenzo mbalimbali za kumwezesha mwananchi kupata uelewa wa jambo hili nyeti na la kihisitoria. Mojawapo ya nyezo hizo ni pamoja na:

a) Kugawa vipeperushi na machapisho mbalimbali yahusuyo Katiba,

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

b) Kugawa vitabu kama Randama, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Bango Kitita, na Rasimu ya pili ya Katiba.
c) Kugawa memory cards, flash, DVD na CD zilizorekodiwa rasimu ya pili ya Katiba
d) Kuonesha filamu yenye maudhui ya Katiba
e) Kufanya mikutano ya hadhara kwa kufundisha na kuruhusu maswali, maoni n.k

Ndugu wanahabari,

Kampeni hii Gogota kwa awamu ya pili ililenga kuzungukia mikoa ishirini ya Tanzania na Zanzibar.

Mikoa iliyotembelewa kwa awamu ya pili inajumuisha mikoa ya Arusha, Tanga, Kagera, Geita, Mwanza, Simiyu, Mbeya, Rukwa, Kilimanjaro, Manyara, Katavi, Iringa, Mara, Njombe, Ruvuma, Pemba Kaskazini, Kusini Pemba, Mjini Magharibi, Unguja Kusini na Unguja Kaskazini. Ndugu wanahabari ifahamike kuwa kwenye kila mkoa tulitembelea wilaya zote na kila wilaya tumetembelea kata tatu na pengine hata zaidi ya kata nne.

MAFANIKIO

Ndugu wanahabari,

Kampeni hii Gogota kwa awamu ya pili, imefanyika kwa mafanikio makubwa, yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana kutokana na awamu hii ya pili ya Gogota:

i. Kuweza kufika wilaya zote za mikoa ishirini iliyokusudiwa, kila wilaya kutembelea kata tatu ni mafanikio makubwa sana ambayo tangu shirika lianzishwe halijawahi kufanya jambo kubwa namna hii. Kwa mara ya kwanza tumeweza kuwafikia watanzania wa mikoa yote kwa pamoja.
ii. Kuungwa mkono na watanzania wengi. Kampeni hii Gogota imekubalika na kuungwa mkono na watanzania kwa kiasi kikubwa sana. Hii imejidhihirisha kupitia umati mkubwa wa watu waliokuwa wakijitokeza kwenye mikutano tuliyoifanya, watu kuuliza maswali na pia watu kutoa maoni na mapendekezo yao. Na wengine kudiriki kutukaribisha kila kijiji na kila kata na hata taasisi mbalimbali kama makanisa, vyuo na shule kutuunga mkono kwa kiasi kikubwa na hata kudiriki kuanzisha programu zinazohusu Katiba.
iii. Kufanikiwa kurudisha agenda ya Katiba kwa wananchi na Uelewa wa rasimu ya pili ya Katiba. Watanzania wengi hasa wale tuliofanikiwa kuwapitia wamepata uelewa

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

mkubwa kuhusu mchakato wa Katiba mpya, pia wamehamasika na kupata ufahamu juu ya zoezi lililobaki la kupiga kura ya maoni. Uelewa huu unapimwa kwa vigezo vingi mojawapo ikiwa ni pamoja na wananchi kupiga simu redioni, kuuliza maswali mikutanoni na kuhamasika na kutaka machapisho mbalimbali ya kujisomea.

iv. Tumefanikiwa kugundua kuwa wananchi wanakerwa sana na jinsi mchakato unavyokwenda hususani suala la Bunge la Katiba kutaka kuchakachua maoni yao yaliyokusanywa na iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

CHANGAMOTO

Ndugu wanahabari,

Licha ya kwamba Kampeni yetu ya kusambaza uelewa wa rasimu ya pili ya Katiba kwa wananchi, imefanyika kwa mafanikio makubwa, tulikutana na changamoto. zifuatazo hapa chini ni baadhi ya changamoto hizo:

a) Uelewa mdogo kuhusu mchakato wa Katiba mpya kwa watanzania wengi. Kampeni hii imebaini kuwa watanzania wengi na hasa walio pembezoni hawana kabisa uelewa kuhusu mchakato huu wa kutengeneza Katiba mpya. Hali hii inazua hofu kuwa hata wakipelekewa rasimu itakayopendekezwa kama watakuwa tayari kuipitisha hata kama si ile ambayo imetokana na Tume ya Mabadiliko ya Katiba yenye maoni ya wengi. Tumebaini kuwa wananchi wengi hasa wa vijijini wanakosa fursa ya kufuatilia mchakato wa Katiba mpya kwa sababu mbalimbali kubwa ikiwa ni kukosa nyenzo kama vile umeme, televisheni, redio na nyinginezo. Kwa mfano katika Wilaya ya Ngara inasikika vizuri redio moja tu iitwayo Redio Kwizera.

b) Umangimeza wa baadhi ya viongozi. Kumekuwepo na viongozi ambao aidha kwa manufaa yao, maslahi ya chama chao, utashi wao au kwa kushawishiwa walikuwa tayari kukwamisha Kampeni yetu ya kusambaza uelewa wa rasimu ya pili ya Katiba kwa wananchi.

Viongozi waliojaribu kutukwamisha katika kazi hii ni;

i. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Ndugu Leonidas Gama
ii. Mkuu wa Mkoa wa Kagera Capt. Fabian Masawe
iii. Kaimu OCD wa wilaya ya Ngara ndugu Paschal Nkuba
iv. Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe Mkoa wa Geita – Ndugu Tajiri

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

v. Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Eng. Stella Manyanya.

vi. Viongozi mbalimbali wa Serikali Zanzibar. (Mkuu wa Mkoa wa mjini Magharibi na wakuu wa wilaya na Masheha wa Mjini magharibi.)

Viongozi hawa kwa nyakati tofauti walikuwa wakizuia mikutano isiendelee na wakati mwingine kutoa vitisho kwa wawezeshaji wa Kituo. Hali hii siyo ya kuruhusu iendelee kamwe, kwani kwa kufanya hivyo ni kuzidi kuwaruhusu viongozi wetu wazidi kulewa madaraka na kushindwa kabisa kuwahudumia wananchi. Hivyo basi Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinazidi kutoa wito kwa viongozi hao waliojaribu na hata kutaka kuzima zoezi letu la kusambaza uelewa wa rasimu ya pili ya Katiba kwa wananchi kuacha tabia hizo, kwani ni kinyume na sheria na haki za binadamu. Ni vema wakatambua kuwa uhuru wa maoni na hata uhuru wa kukusanyika ni uhuru wa kikatiba. Hivyo kwa kujaribu kupokonya haki na uhuru huu ni kuwakosea watanzania na nikujidhalilisha kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo kuna viongozi waliotoa ushirikiano wa hali ya juu na tunapenda kuwapongeza sana kwa hilo. Viongozi hao ni;

i. Inspekta Generali wa Polisi, IGP Ernest Mangu
ii. Mkuu wa mkoa wa Njombe, Capt. Aseri Msangi
iii. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Eng. Evarist Welle Ndikilo
iv. Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Dr. Rajabu Mtumwa
v. Maafisa watendaji wa Kata zote tulizotembelea
vi. Maafisa watendaji wa Vijiji tulivyotembelea
vii. Wakuu wa Shule za Rugambwa, Nyakato, Bukoba Lutheran School – Kagera
viii. Mkuu wa Mkoa wa Iringa Dk. Christine Ishengoma
ix. Wakuu wa wilaya zote za mkoa wa Mbeya
x. OCD wote wa wilaya za mkoa wa Mbeya
xi. Mkuu wa chuo cha Maketikista Makalala A, Mafinga na chuo cha Ustawi wa Jamii, Ruaha- Iringa
xii. Viongozi wa makanisa ambao walioturuhusu kufundisha waumini wao.

c) Mfumo dume kwenye jamii ambapo wanawake wametwishwa mizigo ya kazi nyingi sana kiasi cha kushindwa kushiriki mikutano. Hali hii imejitokeza bayana kwenye

Board of Directors:
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

mikutano tuliyokuwa tukitoa elimu ya Katiba, na hata akina mama walipofika kwenye mikutano wengi wao kama siyo wote walibaki kuwa wasikilizaji tu, tofauti na wanaume waliokuwa wakishiriki kwa kuuliza maswali na kutoa maoni yao. Hali hii ya mfumo dume ni ya kupingwa kwa juhudi zote, na kuzidi kupigania haki na usawa kwa wote. Kwani kwa kufanya hivyo ni kutoa fursa sawa kwa wote na pia ni njia sahihi ya kukuza na kupanua demokrasia nchini.

d) Kutokujua kusoma na kuandika kwa baadhi ya wananchi walioko vijijini. Kampeni hii imebaini kuwa bado watanzania walio wengi hawajui kusoma na kuandika. Hali hii ilijibainisha kwa watu hao kukataa machapisho kwa kigezo cha kutokujua kusoma na kuandika. Hali hii pia inatia hofu hasa utakapofika wakati wa kupiga kura ya maoni, kuwa kutakuwepo na uwezekano wa watu kuambiwa tu kuchagua kile ambacho siyo chaguo lao sahihi. Kwa hali kama hii Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinashauri kuwa serikali itenge muda wa kutosha wa kutoa elimu kwa wananchi hasa wa vijijini kuhusu namna na jinsi ya kupiga kura ya maoni.

e) Hofu ya kutokupata Katiba mpya kwa wananchi. Tuligundua kuwa watanzania wengi wamekata tamaa ya kutokupatikana kwa Katiba mpya. Hofu hii kwa watanzania inatokana na sababu zifuatazo, moja kutokuwa na imani na Tume ya Uchaguzi itakayosimamia zoezi la kupiga kura ya maoni; pili ni Bunge Maalum la Katiba kuacha kujadili rasimu iliyopendekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kujadili rasimu wanayoijua wao; tatu ni kuwepo mgawanyiko kati ya wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba na nne ni kutokuwepo kwa maridhiano.

Ndugu wanahabari,

Kwa kuhitimisha, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinazidi kuwaomba na kuwahamasisha watanzania wote kuzidi kuwa wamoja na kujikita katika kufuatilia kwa karibu mchakato huu wa kutengeneza Katiba mpya. *Katiba ni yetu Taifa ni letu sote tuhusike!.*

Asanteni kwa kunisikiliza,

.....

Dkt. Helen Kijo-Bisimba

Mkurugenzi Mtendaji.

Board of Directors:

Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.